



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

SECOND ASSEMBLY –THIRD SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 20th March 2019

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9:30 a.m.*

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

MOTION

TERMINATION OF SERVICES FOR ALL CASUAL WORKERS WITHIN THE COUNTY PUBLIC SERVICE

Hon. Mwayaa: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I have a Motion to move and it reads as follows:-

That, aware that Section 74 of the County Governments Act, 2012 provides that the County Public Service Board shall regulate the engagement of persons on contract, volunteer and casual workers, staff of joint ventures and attachment of interns in its public bodies and offices.

Aware that, the County Public Service Board has not yet submitted to the County Assembly the regulations for the engagement of persons on contract, volunteer and casual workers, staff of joint ventures and attachment of interns in its public bodies and offices for approval.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Noting with concern that, County Chief Officers have engaged persons on contract and casual basis with neither their knowledge nor guidance from the County Public Service Board nor approved regulations by the County Assembly.

This county assembly urges the County Secretary to direct all the County Chief Officers to terminate services of all casual workers within the County Public Service Board with an exception of casuals from all dispensaries until the County Assembly approves the regulations for engagement of persons on contract, volunteer and casual workers, staff of joint ventures and attachment of interns in the county public bodies and offices.

As the Majority Whip of this assembly, I have decided to bring this Motion to the Floor of this House mainly because Kilifi County needs healing and if the healing is to come then all casuals must be terminated.

Hon. Mramba: Point of Order!

(Hon. Mramba stood on a Point of Order)

The Speaker: What is your Point of Order hon. Mramba?

Hon. Mramba: I need a clarification from you Mr. Speaker. The hon. Member for Kayafungo is saying that as the Majority Whip of this assembly he has decided to bring this Motion to the Assembly. Has he brought this Motion as a Member for Mwanamwinga or as the Majority Whip?

(Hon. Kenga stood on a Point of Order)

Hon. Kenga: The hon. Member for Kakuyuni is misleading the House that hon. Mwayaa is from Mwanamwinga, yet he is from Kayafungo.

The Speaker (Hon. Kahindi): The implication that when you say that I bring this in my capacity as the Majority Whip it might intend to mean that it is a party Motion; that is the only slight difference otherwise it is still okay. The Motion which was approved was signed by hon. Mwayaa, the area MCA of Kayafungo.

Hon. Mwayaa: I will not argue more on the Majority Whip; but still I am a Member of Kayafungo and again I am the Chief Whip of this Assembly. I have brought this Motion as a Member of Kayafungo Ward. Kilifi County needs healing and if Kilifi County is to get the healing then all casuals must be terminated.

The County Government of Kilifi has a huge wage bill and sometimes we do very little for our community because of the wage bill; this is the plight we are facing. You will find that in terms of projects we are doing very little for the community and we have realized that it is because of the casuals that are working in some Departments in Kilifi County. You will find that these casuals were hired without following the rightful procedure. I have a list with me here that the Department of Water and Natural Resources has about 478 casuals and quarterly they have consumed Kshs. 17.813 million that is from October and December. So if you multiple by four which makes one year you will find that a lot of money in Kilifi County goes to paying the casuals. I have a list of about 23 casuals from the Enforcement Department; these were recently recruited with no due proper process. So I want to urge this House to join hands with me so that this Motion can see the light of the day. With those few remarks, I want to call upon hon. Mramba to second.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Hon. Mramba seconded)

(Question proposed)

Hon. Hassan: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Nimesimama kupinga Hoja hii. Sababu za kupinga ni kwamba nafikiri ingekuwa bora kama tutashindwa kutengeneza nafasi za kazi basi ni afadhali tuseme; twapitisha Hoja ya kwamba watu wasiajiriwe tena mpaka bunge la kaunti litoe ruhusa. Ni mambo la kusikitisha kwa sababu sote tunafahamu kwamba kupata kibarua ni kazi ngumu.

Leo hii mtu ana familia asimamishwe kazi wakati wengine wana wagojwa ambao wanawashughulikia. Mimi binafsi sioni kama hili litakuwa ni swala la busara. Hii Nyumba kazi yake kubwa ni kupunguza mambo yanapokuwa moto si kuongeza cheche. Tuko na vijana wengi sana ambao hawana shughuli za kufanya leo hii sisi tunatakikana kuunda kazi lakini si kwenda kuharibu kabisa. Mimi nimesimama na ninapinga tena kwa nguvu zote hii Hoja iliyoko mbele yetu. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Ndago.

Hon. Ndago: Asante sana mheshimiwa Spika. Kwanza nasimama kuunga mkono Hoja hii. Kulingana na vile mheshimiwa Mwayaa amezungumza ya kwamba pesa nyingi za serikali ya Kilifi zinatumiwa kuwalipa mishahara wafanyikazi haswa wa vibarua. Tukiwa Kirinyaga kwa mambo ya ugatuzi, mheshimiwa Rais alisema serikali za ugatuzi nyingi zinatumiwa pesa za serikali ya kitaifa nyingi kulipa mishahara kuliko kuleta maendeleo kwa jamii. Nataka niamini ya kwamba serikali ya Kilifi ni mojawapo; ikiwa idara moja iko na wafanyikazi 478 na tuko na idara zaidi ya 10 mheshimiwa Spika na hakuna mfanyikazi anayelipwa chini ya 10,000; hizo ni pesa nyingi sana ambazo zinaenda kwa mishahara. Mbali na kwamba pesa nyingi zinaenda kwa mishahara, kunao wafanyikazi ambao wameandikwa kwa njia ambazo si za sawa.

Mwenyekiti ambaye anasimamia maswala ya maji na mazingira mheshimiwa Hassan ambaye ametoka kuzungumza kabla mimi nizungumze anajua kwamba wizara ambayo anaisimamia yeye imepeana mwelekeo ambao si mzuri. Sisi kama serikali tunajua ya kwamba wizara hiyo imekosea mambo mengi. Kwanza, ukiangalia wizara hiyo wafanyikazi ni wengi; tumeitengea pesa nyingi tena wamechukua kazi wakapeana kwa mwanakandarasi. Mwanakandarasi yualipwa zaidi ya milioni moja kwa mwezi, na sisi kama serikali tumenunua lori la kukusanya takataka na lori hilo bado linalipiwa na ni la serikali ya kaunti. Mwanakandarasi ana wafanyi kazi wake sehemu ya Malindi...

(Hon. Hassan stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Hassan what is your Point of Order?

Hon. Hassan: Mimi naona mheshimiwa anayezungumza kwa sasa anakosa mwelekeo kwa sababu kama ni idara ambayo naisimamia mimi kama mwenyekiti imepewa majukumu mengi sana kutoka kwa idara nyengine lakini si kwa sababu eti iko na mzigo kutokana na hiyo idara yake. Labda angetoa ufafanuzi na kama ni jambo kuhusu mishahara kuna wafanyikazi sisi tuliwarithi kutoka kwa serikali za zamani za *County Council* na hapo ndio tumeongezekewa na huo mzigo. Kwa hivyo, labda ana ufafanuzi mzuri zaidi anieleweshe. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Ndago?

Hon. Ndago: Thank you, hon. Speaker. Let me speak in English because I want to believe that hon....

The Speaker (Hon. Kahindi): No, your Swahili is very fluent and we would wish you to proceed according to the rules.

Hon. Ndago: Asante sana mheshimiwa Spika. Nataka niamini ya kwamba mwenyekiti wa kamati ambayo leo hii inafanya serikali ya Kilifi leo itatingisha Kilifi nzima kwa sababu yeye mwenyewe ana ufahamu; ni juzi tu kila kamati iliweza kukutana na mawaziri wake. Labda awe hakuhudhuria vikao vyake lakini zile pesa zilizotengwa kununua lori la kuzolea taka ni zaidi ya milioni 21 mheshimiwa Spika; ili kununua lori la kuzolea taka Kaunti ya Kilifi. Milioni 21 ni pesa nyingi sana; tena hapo serikali ikarudi kuandika vibarua. Vibarua ambao wako Kilifi ni 478; wale wanaofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hapa uko na lori na hapa uko na vibarua na hili lori ni la kufanya *recycling*; vibarua ambao uko nao ni zaidi ya 300. Tena tukirudi hapo mheshimiwa Spika bado tuko na vibarua ambao wanalipwa na serikali ya kaunti na wizara ikiwa bado ni moja. Akiwa yeye kama mwenyekiti anafaa kupeana mwongozo hapa ndani ya hawa waheshimiwa na hana mwongozo badala yake anaomba mwongozo kutoka kwa serikali, hafai kuwa mwenyekiti wa hii kamati...

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, proceed with your submissions now.

Hon. Ndago: Kwa sababu serikali inapoteza pesa nyingi na tumechoka kupoteza pesa. Huu Mswada haujaletwa na mtu ambaye yuko nje ya serikali; mheshimiwa Spika Mswada huu umeletwa na mtu ambaye yuko ndani ya serikali nay eye ni Kiranja wa Bunge la Kilifi. Yule ambaye ameunga mkono anatoka upande wa serikali na anayezungumza ni makamu wa walio wengi katika Bunge la Kilifi. Hiyo ni kuonyesha ya kwamba serikali imelemewa mahali fulani. Na ikiwa tumelemewa ni lazima tutafute mbinu ambayo tutaweza kusaidia jamii ya watu wa Kilifi. Na kumsaidia mtu wa Kilifi, tusingojee matamshi kutoka kwa mheshimiwa Rais ya kwamba kunazo kaunti ambazo zimetumia pesa kulipa mishahara; ikiwa Kaunti ya Kilifi ni moja wapo.

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Kombe (Mwarandu) what is your Point of Order?

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, hapo mbeleni tulivyokuwa bado tunasoma katika shule za misingi tuliambiwa kwamba Kiswahili kitukuzwe, kuna tofauti ya makamu na naibu wa walio wengi Bungeni. Sasa Mjumbe wa Shimo la Tewa anapotosha bunge hili kwa kusema yeye ni makamu. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, thank you. Hon. Ndago...

Hon. Ndago: Asante sana mheshimiwa Spika...

The Speaker (Hon. Kahindi): Just to quote, are you a *makamu* or *naibu*?

Hon. Ndago: Mimi ni naibu...

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, proceed.

Hon. Ndago: Mheshimiwa Spika, kunao waheshimiwa ambao wamekuja kutatiza shughuli na kuna waheshimiwa ambao wamekuja kusaidia watu wa Kilifi. Wale waliokuja kutatiza sisi hatuko pamoja na wao; wale waliokuja kusaidia mtu wa Kilifi mimi nitawaunga mkono moja kwa moja. Nikizungumza hivyo ni kwamba naunga mkono Mswada ambao umeletwa kabla tuende kwa Bajeti. Ukiangalia vizuri mshahara wa mtu ambaye amechukuliwa na serikali ya kaunti na hana barua, tunajuliza mshahara wake utatoka wapi? Hilo ni la kwanza.

Hawa vibarua wa Serikali ya kaunti tokea wachukuliwe bila barua kufikia sasa huwezi kufahamu kama ni mtu anafanya kazi na serikali ama ni mtu yuko tu hohe hahe kwa sababu

gani? Mshahara wake huyu mtu unatoka wapi? Na tukipitisha bajeti hakuna mahali tumeweka mshahara wa kibarua. Ndiposa mimi naunga mkono kuhakikisha ya kwamba vibarua wote wakae pembeni na tume ya kuajiri watu kazi iseme tuna upungufu fulani na upungufu huu tunaomba kuchukua watu ili tukawapatie kandarasi, aidha ni ya mwaka mmoja, miaka miwili, mitano ndio hawa watu tuweze kufanya nao kazi.

Mheshimiwa Spika mimi ninashukuru kwa fursa hii kwamba nimezungumza ule ukweli kutoka upande wa serikali ya kwamba mzigo umetulemea na tunataka kupunguza huu mzigo kwa niaba ya watu wa Kilifi na nitakapopata nafasi nitazungumza tena kwa sababu kiongozi wa walio wengi bungeni hayupo; ni mimi nimeshikilia usukani. Nitazungumza kwa niaba yake wakati wowote mheshimiwa Spika utakaponipa nafasi. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): This is getting interesting, Yes hon. Baya.

Hon. Baya: Thank Mr. Speaker, Sir. I wish to congratulate the hon. Senior (Mwayaa) the MCA Kayafungo Ward. Today it has been proved that a short man is always wise...

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Kombe Mwarandu, what is your Point of Order?

Hon. Mwarandu: The hon. Member on the Floor hon. George Baya Mramba, the MCA for Watamu Ward, if I can use a good word then the hon. Member is turning to be senile because it is just yesterday he brought a Statement in this House that the casuals at the Scholarship Board to be absorbed and today he is supporting their contract to be terminated. I think he is more confused than a hon. Member.

The Speaker (Hon. Kahindi): That word is not appropriate; I would like to protect the Member.

Hon. Mwarandu: I will replace that with senile; he is senile.

Hon. Baya: Thank you Mr. Speaker. I think the hon. Member should go back to the Statement and read clearly if he does not understand English.

The Speaker (Hon. Kahindi): Kindly proceed, you are protected hon. Member.

Hon. Baya: Mr. Speaker, I repeat that today we have proved that a short man is always wise bringing this Motion. As the Chairman of Public Investments and Accounts Committee, the few financial reports that I have gone through I have seen that the County Government of Kilifi is spending higher percentage on recurrent expenditures; 80 percent of our recurrent expenditure included inside is the wage bill. Wages are very high and if this County Government is of the spirit of devolution and if this Motion goes through will assist this County Government to reduce its recurrent expenditure and raise the development amount so that it can assist us to fulfill the spirit of devolution.

Mr. Speaker, I know very well as leaders we have promised our voters that we are going to empower them through employment and all that; but there are so many ways of empowering our youths. Now the County Government has introduced the Mbegu fund; this is also a way of empowering our youth instead of unnecessary appointments of these casual workers.

In fact the Department of Environment has been misusing this opportunity in my area; I have few youth who are working at the Environment Department and what is happening is that someone who wakes up around six and by around 9 he is back at home saying he has completed his duty and the same person is expecting a salary at the end of the month. So this opportunity has been misused for long and the only solution is to pass this Motion and terminate all casual workers and find other ways of empowering the youths and also other ways of solving this

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

problem of garbage. I am planning to bring a Motion in this House so that people should not drop garbage anyhow like the way people are used to, so that we can also keep some garbage sites so that people can drop garbage on collecting sites instead of just dropping anything anyhow and then at the end of the day you are expecting someone to be employed and do the same job. Thank you very much Mr. Speaker, Sir. I support this Motion fully.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Mramba.

Hon. Mramba: Asante mheshimiwa Spika. Nami nasimama kuunga mkono nikisema haya machache. Hoja hii imeletwa kwa nia njema na wala haikuletwa ili kuadhibu mtu yeyote. Lakini ukweli ni kwamba sheria inasema wazi wazi kifungu cha 74 kwamba ile tume ya kuajiri itatengeza mapendekezo wayalete bungeni ili tuyapitishie ndio tujue vibarua wanaajiriwa kwa njia gani. Lakini kwa sasa hakuna mapendekezo yaliyoletwa hivyo basi imeleta mwanya kwa *chief officer* kuleta watoto wao au shemeji zao ama hata marafiki zao aidha wa kike ama wa kiume wanaajiriwa kila siku.

Bwana Spika, ni jambo la kusikitisha kwa sababu hata hivi majuzi kuna afisa mmoja hapa Malindi aliwaachisha kazi vijana ambao wanafanya kazi kwenye idara yake na badala yake akachukua watu wake kutoka kwao akiwemo mmoja wao ni mtoto wake wa kumzaa; kijana yule alifanya mtihani juzi na hajapata majibu ya kidato cha nne na hajapata hata kitambulisho mpaka mshahara unapitia kwenye akaunti ya mama yake. Ni jambo la kushangaza...

(Hon. Kenga stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Stanley Kenga, what is your Point of Order?

Hon. Kenga: Thank you, very much Mr. Speaker. The statement which is coming from the seconder of the Motion is something very weighty and I would wish that the same is substantiated that we are able to know the name of the said officer and even to prove that it is very correct that a child of the same person is employed yet this child is an underage; a person with no identification document so that it can be used as a proof of the ills that have bedeviled the department and the entire county. So I would wish you direct the Member to even go further and name this officer for us to be able to know.

The Speaker (Hon. Kahindi): I think that is really a valid point to note because if what hon. Mramba has said is true then we have a very big problem. Do you have any information with regards to the particulars you are talking about or you are using it as a persuasive measure to persuade Members?

Hon. Mramba: Hapana, yule afisa yuko na yule mtoto yuko ingawaje siwezi kupata jina kwa sasa lakini nikipatiwa mda naweza kuleta jina la yule kijana wake. Haya ni maswala ambayo yanaonekana wazi na hawa vibarua pia wamekuwa wakidhulumika sana mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, I direct that you get that name and the name of the kid so that you table them before the Labour Committee for investigation.

Hon. Mramba: Sawa asante. Nikiongezea...

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Humphrey Mwarandu, what is your Point of Order?

Hon. Mwarandu: Asante mshimiwa Spika. Neno hili la “nikipewa mda zaidi”, limekuwa neno sugu kwa mshimiwa wa Kakuyuni...

The Speaker (Hon. Kahindi): No! I have given my direction on the same; you cannot even make a comment...

Hon. Mwarandu: Mshimiwa Spika, unakumbuka...

The Speaker (Hon. Kahindi): Order! Order! I have given my directions...

Hon. Mwarandu: Lakini mshimiwa Spika...

Hon. Mramba: Mshimiwa Spika...

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Humphrey (Mwarandu), do not make me invoke Standing Order 105. Hon. Mramba has made a statement. Our Standing Orders demand that if a Member rises up to ask you to substantiate, then if you are not able to do so at that particular time, then a time is given. My directions are, and the Chairperson Labour I think he's walked out; that the Vice Chairperson, kindly take up that matter because it's a matter that requires investigations and if you invite hon. Mramba to appear before your committee so that he tables that information, then you take it up. That is the ruling and that matter is closed. Yes proceed. Yes hon. Kenga, are you rising on a Point of Order or a Point of Information?

(Hon. Kenga stood on a Point of Order)

Hon. Kenga: Mr. Speaker it's on a Point of Order. I am rising because hon. Mramba has requested for time to be able to table before this Assembly and it's very much in order but he has only told us that the name of the kid who was employed is what he does not have but the name of the officer is with him. So I request that he goes ahead to tell us who the officer is as we wait for the name of the kid.

Hon. Speaker (Hon. Kahindi): Is that what you said hon. Mramba?

Hon. Mramba: Mshimiwa Spika, nitaleta jina la yule afisa pamoja na mtoto wake aliyemuajiri.

Hon. Speaker (Hon. Kahindi): There will be consequences. Hon. Shaban you will need to report to us within 14 days that you have called hon. Mramba and he's been able to give you that information. If he will not have been able to give that information then the Chairperson or the Vice Chairperson will report to this House that hon. Mramba was only bluffing and then the Speaker will make his direction.

Hon. Mramba: Basi Mshimiwa Spika nikiendelea ni kwamba, hawa vibarua ambao wameajiriwa na Kaunti yetu kama alivyoongea naibu wa kiongozi wa walio wengi, ni kwamba hapa kuna malori ambayo yamekodishwa kutoka kwa mtu binafsi ambayo kwa mwezi moja yule bwana analipwa inakaribia milioni moja; hilo lori liko na wafanyikazi na linazunguka kuokota taka halafu mwisho wa mwezi linalipiwa shilingi milioni moja. Hapa tuko na wafanyikazi zaidi ya 400 ambao wameajiriwa kwa idara moja peke yake. Hawa wafanyikazi ambao ni vibarua wanadhulumika kwa sababu wanakatiwa pesa za NSSF na NHIF na hizo pesa haziendi kule kwa hivyo zinakatwa kwa *payslip* zao lakini pesa haziendi, na hatujui zinapotelea wapi. Labda mweynekiti wa kamati ya *Labour* pia nalo ulichunguze.

Zaidi ya hapo ni kwamba kila mwisho wa mwezi wale vibarua wanatia sahihi kuhakikisha malipo yao ya ule mwezi na siku alizofanya kazi. Atatia sahihi ya 15,000 kwa mfano, akifika benki anakuta kuna 12,000. Kuna *deduction* ya 3000 ambazo hazijulikani zinaenda wapi kila mwezi. Hapa Mshimiwa Spika, hili jambo mbali na kuwasimamisha kazi, uchunguzi ufanyike kupitia kwa kamati tuone hizi pesa zao zinaenda kwa mifuko gani. Kuna

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wakati tulikuja tukakaa na Bodi tukawauliza na wakasema hawajaajiri kibarua hata mmoja lakini *Chief officers* wanaajiri watu wao kila siku.

Leo katika gazeti la *The Star* tumesoma kwamba Kaunti ya Vihiga imesimamisha mishahara ya vibarua kupitia kwa benki kwa sababu wanasema kuna majina mengi yako tu kwa *payroll* lakini hawajulikani wako wapi; pengine wako majumbani wanaenda tu kuchukua mishahara na kurudi nyumbani. Wakasema wamesimamisha na kibarua atakuwa akichukua mishahara *cash* kwa ofisi ili kuzuia hii mianya ya pesa nyingi kupotea.

Tumeona pia Mheshimiwa Rais akisema kwamba Kaunti nyingi zinatamia pesa nyingi kwa mishahara kuliko maendeleo. Kaunti ya Kilifi tunakaribia 70% kwa mishahara peke yake; maendeleo yanaenda karibu 30% peke yake ambayo hio si haki. Hii kaunti ilikuja ilete maendeleo kule chini kwa wananchi wala haikuja kuleta mahali ambapo kunaweza kuajiriwa ndugu zangu au rafiki zangu. Ninachoomba mheshimiwa Spika ni wale vibarua wasimamishwe sio kusimamisha hawa wa idara moja ya mazingira peke yake maanake tunaona wengi waliosimamishwa mwezi huu ni wale wa Idara ya Mazingira. Tunataka wote kwa kila idara kama kuna kibarua hata kule kwa *scholarship* kama Mheshimiwa George Baya alisema wao pia wasimamishwe. Halafu wakisimamishwa tuje tukae na bodi ndio tujue mipangilio ya kusaidia wale vijana; aidha kama watarudi au hawatarudi lakini angalau tuwe tumewasaidia kuwapatia ajira ambayo itawasaidia hata mbeleni. Kwa hayo naomba kuunga mkono. Asante.

Hon. Speaker: Hon. Shaban.

Hon. Shaban: Asante Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Mswada huu. Nataka kumshukuru Mjumbe wa Kayafungo kwa kuleta Mswada huu. Hapa Kaunti ya Kilifi tuko na shida kubwa sana ya vibarua. Nataka nikupatie takirimu kidogo Mheshimiwa Spika ndio tuweze kujua vibarua ni wangapi katika Kaunti ya Kilifi. Katika Idara ya Uगतuzi tuko na vibarua 57, katika Idara ya Afya tuko na vibarua 768 na katika Idara ya *Trade* tuko na vibarua 10.

(Hon. Ndago stood on a Point of Order)

Hon. Ndago: Thank you, Mr. Speaker. Kindly can the hon. Member Shaban clarify to the hon. House whether he is giving facts because I want to believe that he is the Deputy Chairperson of the Labour Committee and the Chairperson is not around? Is he giving out the information that this is what should be done out of supporting the Motion? What he is actually giving out is the records from the departments and I think as a committee, looking in this House Mr. Speaker the two Chairpersons have run away; Chairperson for Labour and the Chairperson for Water and Natural Resources. Whatever hon. Mwayaa has brought to this House I want to believe that those are the facts. Hon. Shaban should not be used by the other side. He shouldn't speak on behalf of the Executive.

Hon. Speaker: He is actually speaking in support of the Motion.

Hon. Ndago: No, but he is giving out some points. I want to believe that these are the expectations of not less than 20 or 10 Members that hon. Shaban is the Deputy Chairperson of the Labour Committee and as a Deputy you must know before this Motion came to this hon. House. They were supposed to tell us in the Committee's that we have this problem; then we as Members come out and decide.

(Hon. Mramba stood on a Point of Order)

Hon. Mramba: Mr. Speaker, I am meant to believe that hon. Ndago is confusing the whole Motion Mr. Speaker because hon. Shaban was giving us the details so that we can know the magnitude of this problem. So I think he was in order.

Hon. Speaker: Order! I want to protect Hon. Shaban; I presuppose that he will table that document. I believe it's a document that is genuine by virtue of him being the Vice-Chairperson of the Labour Committee; it is my assumption that you have the contents with you. You will proceed to give us the overview of what is really happening at the Executive. We have a point of order from hon. Mwarandu. What is your Point of Order?

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, nitaregelea tu palepale kwa Kiswahili kitukuzwe. Alivyokuwa anaongea mbele ya Bunge hili mheshimiwa Dickson Shaban amesema kwamba ako na takirimu na Kiswahili sanifu ni 'takwimu'.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you for the correction, *mwalimu wa Kiswahili*. Proceed hon. Shaban.

Hon. Shaban: Asante mheshimiwa Spika, ameniambia ni twakimu. Nafikiri ndugu yangu mheshimiwa Ndago ambaye pia ni jirani kule Mtwapa alikuwa hajanielewa vizuri. Mimi ni Naibu Mwenyekiti wa Kamati ya Leba na nimesimama kuunga mkono kwamba hawa vibarua waweze kuondolewa. Ndio maana nikasema kwamba wakati Mswada ukija ni jukumu langu kama mheshimiwa nikija katika sakafu hii kuchangia ni lazima niwe nimeipitia na nimetafuta habari ili niweze kuizungumzia.

Ndio maana nikasema kwamba katika Idara ya Ugatuzi iko na vibarua 54, Idara ya Afya 769, Idara ya Biashara 10, Idara ya Ukulima 25, Idara ya Mazingira 422, Idara ya *Executive* 20, Irada ya Elimu 39, Idara ya Teknolojia na Mawasiliano 52, Idara ya Uchukuzi 42, Idara na Idara ya Pesa 51. Kwa jumla tuko na vibarua 1,506; huu ni mzigo mkubwa sana ambao unalemea serikali kama vile ndugu yangu mheshimiwa Ndago alivyosema.

Nakumbuka siku moja tuliweza kumwita Mwenyekiti wa Bodi James Mulewa tukiwa na Kamati ya Leba na tukamuuliza hawa vibarua wanalipwa na kina nani kwa sababu sisi tunajua kwamba wewe ndiye Mwenyekiti ambaye unaajiri watu na kukitokea nafasi za kazi ni jukumu lake yeye kutangaza watu waweze kutuma maombi na baadaye kuchukuliwa. Nataka niseme kwamba Mwenyekiti wa Bodi ile James Mulewa alisema yeye hajui vibarua hao wanalipwa na kina nani.

Ni kwamba vibarua hawa wanalipwa na *Chief Officers* pasipo na mipangilio mizuri ya Bodi. Mimi nataka nisema kwamba tunaunga mkono huu Mswada ili kuwe na nidhamu katika mambo ya kuajiri wafanyikazi. Mfanyikazi ni sharti apewe barua; ni sharti barua yake ielezwe vizuri kwamba yeye yuko katika kandarasi ama kazi ya kudumu. Lakini vile ambavyo tunaona ni kwamba vibarua hawa hawana barua yoyote ya kusema kwamba wameajiriwa. Ikiwa mtu hana barua mheshimiwa Spika ni tatizo kubwa sana kwa sababu huwezi kusaidika kamwe; huna barua huna lolote wewe umekaa tu hivi hivi. Kwa hivyo inafanya ile *wage bill* inapanda juu sana.

Mimi nataka tulate nidhamu katika mambo ya kazi. Watu waandikwe vizuri; ijulikane kama wewe kandarasi yako ni ya miaka mitano, ufanye kazi na baada ya miaka mitano kama kuna marupupu upewe. Lakini vile tunaenda tunaona kwamba huu mzigo ni mkubwa. Naona kwamba mheshimiwa wa Jaribuni ambaye ni mwenyekiti wa Kamati ya Utekelezaji amelalia kazi yake. Tunataka huu Mswada utakapopita uweze kutekelezwa mara moja ili tuweze kuokoa Kaunti ya Kilifi. Asante sana mheshimiwa Spika. Mimi nataka nikomee hapo.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Hon. Mramba stood on a Point of Order)

Hon. Mramba: Mr. Speaker, hon. Dickson Shaban is raising a very pertinent issue in regards to the conduct of the Chairperson of Committee on Implementation. I would rather he apologies or he brings a substantive Motion to discuss the conduct of the Chairperson. It is not fair.

The Speaker (Hon. Kahindi): I think that is noted. As to whether or not the Chairperson is doing his job or not, I think that is a matter that is supposed to be discussed at the Liaison Committee not to be brought here without any substantive evidence. It is demeaning to raise a statement like that. I do not think it is fair to say somebody has failed without justification. I would wish you withdraw that statement.

Hon. Shaban: Mheshimiwa Spika, unajua hii inatokana kwamba...

The Speaker (Hon. Kahindi): Otherwise I will require you to bring and table evidence to this House

Hon. Shaban: Mheshimiwa Spika, naomba niondoe maneno hayo. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. Okay hon. Mwarandu. Let us hear you speak in Kiswahili now so that we can learn from you.

Hon. Mwarandu: No I will speak in English.

The Speaker (Hon. Kahindi): Proceed.

Hon. Mwarandu: Thank you very much, Mr. Speaker, for this opportunity. Today I am between the devil and the blue seas and this is because the Mover of the Motion is a very senior Member of this Assembly and not only that but he is my area MCA(Member of County Assembly). That notwithstanding, I think we are all here because of some laws and we are guided by the Standing Orders in this Assembly, that is number one. Number two, we have the supreme law which is the Constitution of Kenya and then we have other statute laws.

Allow me to refer to Standing Order number two of our County Assembly. 'The decision made in paragraph (1) shall be based on the Constitution of Kenya, statute law and the usages, forms, precedents, customs, procedures, traditions and practices of the County Assembly of Kenya and other jurisdiction to the extent that these are applicable to Kenya.' Why am I referring to this Standing Order? It is because passing this Motion is going to be a breach of the Constitution, one, and two the Employment Act.

Standing Order number 87 talks about statements of facts; we cannot deliberate on a Motion here based on hearsay since we cannot ascertain who these casual workers are. I think the Mover of the Motion ought to have done what he did yesterday rather than bringing this Motion before this Assembly. Yesterday he tabled a Statement requesting the list of casual workers first then after that we could now know who these casual workers are.

(Hon. Mwayaa stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Mwayaa you have a Point of Order?

Hon. Mwayaa: Mheshimiwa Spika, mnenaji ambaye yuko kwa Sakafu anasema ya kwamba kuwasimamisha vibarua hawa itakuwa ni kuvunja sheria. Ni sheria gani iliyofanya mpaka vibarua hao wakaandikwa? Manake tunaona ya kwamba waliandikwa bila kujulishwa Bodi na yeye anasema kwamba tutakuwa tumevunja sheria; atuelezee ni sheria gani ambayo tutakuwa tumevunja.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, press your microphone.

Hon. Mwarandu: Thank you Mr. Speaker. Sometimes hon. Members rest their eyes and if they rest their eyes sometimes they also rest their ears. What I have said Mr. Speaker is that we cannot really ascertain or we cannot prove that there are casual workers in this county government because we do not have any list to prove the same Mr. Speaker and if we are going to go by the...

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Mwayaa, what is your Point of Order?

Hon. Mwayaa: Niko na orodha ya vibarua 478 na kama zile *Quarterly Report* tunazozipata hazisomi vizuri, nataka nimtume asome ile *Quarterly Report* iliyotoka kwa Maji; ataona kwamba kuna vibarua pale 478 ambao wamekula pesa yetu ya Kilifi milioni 17. 813. Kwa hivyo, wako vibarua na asipotoshe Bunge hili.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Mwarandu.

Hon. Mwarandu: Mr. Speaker, the only Member who has the list is the Mover of the Motion, right? And that is making it difficult for us to know the authentication of the list; we cannot even know the origin of that list Mr. Speaker. So I still believe that because that list has not even been tabled before this House Mr. Speaker...

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Mwayaa

Hon. Mwayaa: Ripoti hii inayozungumziwa mheshimiwa Spika ililetwa ndani ya Bunge hili na iligawanywa kila Mjumbe ambaye yuko hapa. Kwa hivyo akisema ya kwamba haijaangaliwa nafikiri anaendelea kupotosha zaidi maanake yeye ni Mjumbe ambaye yuko hapa na anastahili kusoma kila nakala ambayo anapatiwa; asiendeleo kutupotosha mheshimiwa Spika. Nakala hii ilijadiliwa hapa.

The Speaker (Hon. Kahindi): Quarterly Reports are normally tabled before this House and deliberated. I am seeing you have a valid point, okay? You were expecting him to perform like the way lawyers do, okay? Because what he has not done and probably which he should have done to easily convince you is that during submissions; you see like the way lawyers do that they say Your "Lordship I relay on this authority" and then you hand it over then you proceed; that is not that. However, in the County Assembly record and I am aware has the Quarterly Reports which indicates the number of casuals which are available in the department because remember him, is only very specific to a particular department from his submissions. However, his Motion requires that all the casual staff be sent away with an exception of the ones in the Health Department. So proceed hon. Humphrey (Mwarandu), if he will not have convinced you it is okay but as to whether or not the numbers are available in the record of the Assembly, they were tabled here.

Hon. Mwarandu: Thank you very much Mr. Speaker. What I was saying is that we are also guided by the supreme law which is the Constitution of Kenya 2010 and Article 236(b) which says that "A public officer shall not be dismissed, removed from office, demoted in rank or otherwise subjected to disciplinary action without due process of the law" Mr. Speaker.

